

HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM



TANGAZO LA NAFASI YA MWENYEKITI WA BODI YA SHIRIKA LA MAENDELEO LA DAR ES SALAAM (DDC)

Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam inawatangazia Watanzania wote hususani wakazi wa Jiji la Dar es Salaam kwamba inahitaji kupata mtu mwenye sifa na uwezo wa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Maendeleo Dar es Salaam (DDC).

SIFA ZA MWOMBAJI

1. Awe raia wa Tanzania, Mkazi wa kawaida wa Jiji la Dar es Salaam.
2. Awe na umri usiozidi miaka 65.
3. Awe na elimu ya Shahada ya Uzamili au katika fani ya Uchumi, Usimamizi wa Biashara na Mipango.
4. Awe na uzoefu wa uongozi katika Taasisi za biashara, uchumi na mipango kwa muda usiopungua miaka kumi na tano (15).

MAJUKUMU

1. Kuongoza vikao vya bodi.
2. Kusimamia shughuli za Shirika kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo ya Serikali.

UJIRA

Malipo ya Ujira yatatokana na posho za vikao vya Bodi.

MAOMBI YOTE YAAMBATANISHWE NA:-

1. Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
2. Nakala ya cheti cha taaluma
3. Maelezo binafsi ya mwombaji (CV)

4. Picha ndogo (Passport size) mbili za hivi karibuni

Barua zote za maombi zitumwe kwa njia ya Posta katika anwani ifuatayo:-

Mkurugenzi wa Jiji,
Halmashauri ya Jiji,
"Ukumbi wa Jiji"
S.L.P. 9084,
1 Barabara ya Morogoro,
11882 DAR ES SALAAM.

Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 15/11/2018



Sipora J. Liana
MKURUGENZI WA JIJI
HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM